JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI

Namba za simu;
Mkuu wa Shule 0622944834
Makamu Mkuu wa Shule 0655808399
Mwandamizi  Taaluma 0752147048

Shule ya Sekondari  Kaitoro,
S.L.P 1937,
BUKOBA.
Tarehe 15.04.2026

Mzazi/mlezi wa Mwanafunzi.............................
…………………………………………………
………………………………………………….

**YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAITORO HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA MKOA KAGERA MWAKA ………………..

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………… na atasoma tahasusi ya…………

   Shule ya sekondari Kaitoro  ipo umbali wa Kilometa 55 magharibi mwa Mji wa Bukoba. Usafiri wa Hiace kutoka mjini Bukoba unapatikana katika kituo cha mabasi Kibeta. Kuja mji mdogo wa Katoro nauli ni shilingi 5,000.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

   **2.1** Sare ya Shule ni:-

   **i.** Suruali mbili nyeusi zenye malinda mawili kila upande, mifuko miwili ya kawaida pembeni, mfuko mmoja nyuma wenye kifungo nap indo la chini (Turn-up). Mapana kwa chini (yaani miguuni) iwe na vipimo vya inchi 16-18. (zisiwe za mitumba)
   **ii.** Mashati mawili meupe ya mikono mifupi (Tetron) yasiwe ya mitumba.
   **iii.** Sare ya Michezo ni (Bukta, T-shirt na Socks) za kampuni ya ADIDAS/SPORTS (T-shirt isiwe na maandishi yoyote tofauti na nembo ya kampuni), pamoja na Raba za michezo vitavaliwa wakati wa michezo uwanjani tu. Rangi ya Bukta, T-shirt na socks inatokana na tahasusi uliyopangiwa kwa mchanganuo ufuatao;-
   **HGK-**Blue, **PCM**-Kijani

   iv. Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi, Dark-blue jozi mbili au zaidi.
   v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali usiwe na Bi-cross pana wala wenye maandishi au picha yoyote.

vi. Sweta moja ya rangi ya kijani jeshi (inapatikana shuleni)
vii. Nguo za kushindia aje na T-shirt mbili za rangi ya gold plain (dhahabu) zenye nembo ya shule nyuma mgongoni, ziwe nzito na ziwe na kola, pia aje na suruali za kitambaa mbili rangi ya Dark-blue kw aajili ya kushindia (sifa ya suruali hizi iwe sawa na kifungu (i) hapo juu).
viii. Tai moja ya rangi ya Light grey yenye michirizi mieupe ya kukatiza kwa mshazari

***NB: Kwa mzazi yeyote atakayepata mkanganyiko juu ya sare zilizotajwa apige simu kati ya namba zilizoorodheshwa ili kupat maelekezo zaidi kabla ya manunuzi ili kuondoa kununua sare isiyo sahihi.***

***Mwanafunzi hatakiwi kuja na shati,suruali, au nguo nyingine zozote tofauti na alizoagizwa(HAZIRUHUSIWI KABISA SHULENI)***

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12 (counter book 4quire)
ii. Ream(A4) ya karatasi, mbili(2) kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (angalia kiambatanisho D)
iv. Scientific calculators (Non programmable)
v. Godoro 1 la sponge size futi 2 na nusu kwa sita
vi. Mashuka jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, mto na foronya ya pinki na chandarua 1
vii. Nguo za ndani za kutosha
viii. Vyombo vya chakula(sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
ix. Ndoo 2 ndogo (Lita kumi) zenye mifuniko
x. Toilet papers za kutosha.
xi. Mathematical set kwa tahasusi za sayansi na Jiografia

MWANAFUNZI AJE NA VIFAA VIFUATAVYO KULINGANA NA TAHASUSI YAKE:

| TAHASUSI | KIFAA |
|---|---|
| PCM | -Kwanja lililonolewa, soft broom, squizer |
| HGK | -Jembe lenye mpini, chelewa, squizer |

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

- **Michango ya shule iliyoorodheshwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya shule namba 0150859280400 katika benki ya CRDB yenye jina SHULE YA SEKONDARI KAITORO.**
  **(Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na kuja nayo shuleni).**

**3. Sheria na kanuni muhimu za shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la uzima;
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation);
- Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani nan je ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule
  Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kutunza mali za shule;
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**MUHIMU**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alipopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na;**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kutofanya mitihani na mazoezi;
iv. Kugoma, kuhamasisha na kuongoza migomo;
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake , walimu/walezi na jamii kwa ujumla
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywajiwa pombe, uvutaji wa sigara na matumizi ya dawa za kulevya kama vile; uvutaji wa bangi , cocaine, mirungi, kubeli nk;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia sim ya mkononi katika mzingira ya shule;
xiv. Kudharau bendera ya Taifa;
xv. Kutofanya adhabu kwa makusudi;
xvi. Kupanga au kuishi mitaani ukiwa shuleni wakati wa masomo;
xvii. Kutenda tendo lolote lisilokuwa la kwaida shuleni au nje ya shule;
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xix. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

TANIBIHI

a) Lazima aje na kadi ya bima ya afya ya mwanafunzi inayotolewa na NHIF(Shirika la Taifa la Bima ya AFYA) au shilingi 50,400/=
b) Cheti kutoka kwa Daktari: inambidi arudishe fomu ilioambatanishwa iambatanishwe ikiwa imethibitishwa na daktari wa Hospitari ya Serikali ya Halmashauri ya wilaya au mkoa kuwa umepimwa na kwamba unaweza kumudu masomo na kzi za nje bila matatizo
c) Aje na **result slip** yake ya kidato cha nne (original na copy moja)
d) Uraia; anatakiwa kuleta shuleni nakala moja ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)
e) **Kukubali masharti ya shule;** Sheria za shule na fomu ya kukubali kutii kwa dhati sherio hizo pamoja na fomu ya maelezo yako binafsi vimeambatanishwa. Mwanafunzi azisome kwa makini sheria hizo, akizikubali, aweke saini yake kwenye fomu ya kukubaki kujiunga mbele yako mzazi, mlezi, pia ajazefomu ya

maelezo binafsi ya mwanafunzi na aziwasilishe fomu hizo shuleni siku ya kuripoti.

f) Abandike picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu pamoja na namba zao za simu wanaoweza kutembelea mwanafunzi na kushirikiana na shule katika malezi.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Julius Nestory Kashubao
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa motto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;-**

- **Mkuu wa shule; 0629447834**
- **Makamu Mkuu wa shule; 0655808399**
- **Mwandamizi Taaluma; 0752147048**

**BUKOBA DISTRICT COUNCIL**

**Kaitoro Secondary School,**
**P.O. BOX 1937,**
**BUKOBA.**
**Date……………………**

**To medical officer**
**…………………………**
**…………………………..**
**………………………….**
**………………………….**

**Ref :………………………………………………………… (Name of student)**

Please examine the above named student as per examination form below:

………………………………
HEADMASTER

MEDICAL EXAMINATION FORM
(**To be completed by Government Medical Officer**)

Full Name:……………………………………………………………………………….
Age……………………Height……….. (cm) Weight……………. (kg)

1. Blood count………………………………………………………………
2. Stool Examination……………………………………………………..
3. Urinary……………………………………………………………………….
4. STDs and other V.D……………………………………………………………
5. TB and Leprosy test………………………………………………………….
6. Eye Test…………………………………………………………………………
7. Ear Test………………………………………………………………………….
8. Chest…………………………………………………………………………….
9. Abdomen……………………………………………………………………..
10. Spleen……………………………………………………………………….

Any additional information:
E.g. Physical defects or impairment, infections, chronic or family diseases (Sickle cell), in ability to eat certain food etc.

……………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………….

I have examined the above named student and I certify that He /She is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

……………………………. ……………………………
Signature and Official Stamp Date
Station…………………….. Designation……………………

KIAMBATISHO B

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili…………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………..
   Anwani ya nyumbani…………………………………………………………..
3. Mahali unapoishi(nyumbani kwenu): Wilaya…………………Tarafa……………….Kata…………..Kijiji…………..
4. Shule ya sekondari ulikotoka…………………………………………………
   Anwani ………………………………………………………………………..
   ……………………………………………………………………………….
5. Dini…………………………………………………………………………..
6. Kabila………………………………………………………………………..
7. Taifa (Mtanzania/si Mtanzania)……………………………………………….
8. Jamaa katika familia: (Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni
   i. Jina la Baba……………………………………………….
      Anwani……………………………Simu Na…………….
      Anaishi/Haishi…………………………………………….
      Kazi yake…………………...…………………………

      Picha ya baba mzazi

   ii. Jina la mama…………………………………………………
      Anwani………………………Simu Na………………….
      Anaishi/Haishi……………………………………………
      Kazi yake…………………………………………………

      Picha ya mama mzazi

   iii. Jina la mlezi…………………………………………………
      Anwani ……………………..Simu Na………………….
      Kazi yake…………………………………………………
      Uhusiano wake na wewe…………………………………

      Picha ya mlezi/ndugu wa karibu

   iv. Jina la mlezi ……………………………………………
      Anwani…………………………Simu Na……………….
      Kazi yake ………………………………………………….
      Uhusiano wake na wewe…………………………………

      Picha ya mlezi/ ndugu wa karibu

   v. Idadi ya kaka……………………………………………..
   vi. Idadi ya dada…………………………………………
   vii. Wewe ni wa ngapi katika familia…………………………

Mimi …………………………………. (Mwanafunzi) nathibitisha taarifa zilizojazwa hapo juu ni za kweli.

………………………….                                        ……………………….

Sahihi ya mzazi/Mlezi                                        Tarehe

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa…………………………………….

Sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa……………………….Tarehe………………

Simu Na:1……………………………2……………………………………..

KIAMBATISHO A

Anwani……………………………
………………………………
……………………………….
………………………………
Tarehe………………………….

Mkuu wa shule,
Shule ya Sekondari Kaitoro,
S.L.P 1937,
BUKOBA.

**YAH: KUKUBALI NA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAITORO**

- Mimi…………………………………………….. (Jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya sekondari Kaitoro kuanzia mwaka………………***Nakubali/Sikubali** nafasi hiyo. Nimesoma na kuelewa sheria na masharti ya kujiunga na shule hii yaliyoambatanishwa. Hivyo ninaahidi kujifunza kadri ya uwezo wangu wote bila kupoteza muda au kufanya mzaha wowte kama sheria zilivyo ainishwa. Nitatimiza wajibu wangu wote kwa muda na wakati uliopangwa. Pia ninaahidi kuwa nitaii sheria zote za shule. Endapo nitashindwa kutii na kufuata Sheria hizo hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi yangu. Natoa ahadi hizi mbele ya Mzazi/mlezi wangu, ambaye naye ametia sahihi yake kwenye kifungu kinachofuata chini.

……………………………….. ……………………………………..
SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

Mimi…………………………………………………….. (Jina la mzazi/mlezi)
*Nakubali/Sikubali mtoto wangu ajiunge na Shule ya Sekondari Kaitoro. Nimesoma na kuelewa sheria na masharti ya kujiunga na shule hii. Hivyo nakubaliana na masharti na sheria hizi ambazo itambii mwanangu azifuate kama alivyoahidi mbele yangu. Nipo tayari kulipa michango yote. Nitashirikiana na uongozi wa shule pamoja na jumuiya nzima katika kutoa malezi bora kwa mwanangu kulingana na sheria za shule na matakwa ya Taifa kwa ujumla.
Taarifa na mawasiliano yote yahusuyo mwanangu yatumwe kwangu kwa kutumia anwani ifuatayo
………………………………
………………………………..
…………………………………
………………………………Namba za simu:…………………….
……………………..
Mabadiliko yoyote ya anwani yangu nitayatuma kwa Mkuu wa shule kwa maandishi
Sahihi ya *Mzazi/mlezi………………………. Tarehe……………..

****Futa isiyotakiwa***

**KIAMBATISHO D**

**ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI**

Mzazi unashauriwa kumnunulia mtoto wako vitabu kwa kila somo analokuja kusoma kama ilivyoainishwa hapa chini.

CHEMISTRY

i. Inorganic chemistry by TIE(Part 1&2)
ii. Physical chemistry Vol1 and II
iii. Physical chemistry by Chand
iv. Organic chemistry by TIE

PHYSICS

i. Advanced level Physics form five by TIE
ii. Advanced Physics 7th Edition by Nelcon & Parker
iii. A level Physics by Rodgers Mancaster
iv. Advanced Physics class xi by S.Chand

GEOGRAPHY

i. Fundamental Geography by Josephat Mwita A.M
ii. Physical Geography by Monk House
iii. Practical Geography for Africa by John Richard

ADVANCED MATHS

i. Advanced level pure Math Vol1 & II by J.K. Backhouse
ii. S. Chand’s Mathematics for class XI by H.K OASS, Dr. RAM VERMA
iii. Advanced mathematics form V & Form VI by S.I.Sillem

HISTORY

i. Advanced level History for form Five and Six by Oxford
ii. Advanced level History paper 1&2 by Z. Kamili
iii. The evolving world by Denis Ngalula

KISWAHILI

i. Kiswahili Kidato Cha Tano(2024) - TIE
ii. Dunia uwanja wa fujo - Euphrase Kezirahabi
iii. Ua la Faraja - W.E. Mkufya
iv. Mirathi ya Hatari - C.G.Mung’ong’o
v. Wasifu wa Siti Binti Saad- Shaaban Robert
vi. Mukwava wa Uhehe -M.M.Mulokozi
vii. Shujaa Mirambo - Emmanuel Mbogo
viii. Usaliti mjini - Francis Imbuga
ix. Fumbo linaloelea - Nyambari C.M.Nyangwine
x. Malenga wa ziwa kuu -Wallah Bin Wallah
xi. Andamo, Msafiri safarini -Mohammed Khelef Ghassani
xii. Wosia wa Baba - Ahmed Mohamed Amanzy